# Mwongozo wa Kisheria Kwenye Vikwazo na Uzimaji Mtandao barani Africa

International Commission of Jurists

Ikiwa na majaji na mawakili 60 kutoka maeneo yote ya ulimwengu, Tume Ya Muungano wa Wanasheria inakuza na kupigania haki za binaadamu kupitia Kanuni za Sheria, kwa kutumia upekee wa tajiriba yake kwa kukuza na kuimarisha mifumo ya kisheria kitaifa na kimataifa. Ilianzishwa mwaka wa 1952 na iko imara katika mabara matano, ICJ inabania kuhakikisha kuwa kuna maendeleo endelevu na utekelezwaji kamilifu wa haki za binaadamu za kimataifa na sheria za kibinaadamu za kimataifa; kulinda uwepo wa haki za kiraia, kitamatuduni, kiuchumi, kisiasa na kijamii; kuweka salama ugawanaji wa mamlaka; na kuhakikisha uwepo wa uhuru wa mahakama na taaluma ya kisheria.

® **Mwongo wa kisheria kwenye vikwazo mtandaoni na uzimaji barani Africa**

© Hakimiliki ya Tume ya Kimataifa ya Wanasheria Aprili 2022

Tume ya Kimataifa ya Wanasheria (ICJ) inaruhusu utoaji wa kipengele zao kutoka machapisho yao yoyote mradi tu kuwe na kuridhia na nakala ya chapisho iliyo na kepengele inatumwa kwa ofisi kuu kupitia anwani ifuatayo:

Tume ya Kimataifa ya Wanasheria
Rue des Buis 3
S.L.P 1740
1211 Geneva 1
Switzerland

Mwongozo huu wa kisheria umechapishwa na ICJ kupitia msaada wa Ofisi ya Masuala ya Kigeni ya Serikali ya Ujerumani. Mwongozo huu ulitayarishwa na Mwanasheria Justice Alfred Mavedzenge. Upitiaji wa mwisho ulifanywa na Ian Seiderman. Mulesa Lumina Uhakiki na kulainisha mswada wa mwisho.

Federal Republic of Germany
Foreign Office

# Mwongozo wa Kisheria Kwenye Vikwazo Mtandaoni na Uzimaji barani Africa

April 2022

**UTANGULIZI**

Kupata mtandao ni muhimu ili kugundua uhuru wa kuzungumza, haki ya kupata habari na kudumisha haki za binadamu nyinginezo zinazohusiana.[1] Hata hivyo, barani Africa, kama ilivyo kote ulimwenguni, mazoea ya uzimaji mtandao kwa nia ya kubana upataji wa habari na upataji haki za kuzungumza umeongezeka sana. Kwa mtazamo wa kutoa kifaa kwa waandalizi wa sera, wataalamu wa kisheria, na mashirika ya kijamii ile kuangazia utendaji ulio kinyume na sheria na bila mwongozo katika eneo hili, Tume ya Kimataifa ya Wanasheria (ICJ) imetengeneza mwongozo huu wa kisheria.

Mwongozo huu umetokana kimsingi kutoka wajibu wa kisheria unaotoka katika *Maagano ya Kimataifa kwenye Haki za Kiraia na Kisiasa* (ICCPR)[2] na *Makubaliano ya Africa kuhusu Haki za Kibinaadamu na Watu* (ACHPR),[3] kama ilivyothibitishwa na kutafsiriwa na Umoja wa Mataifa (UN) na majopokazi na serikali za kikanda.[4] Takribani Nchi zote za Africa ni wanachama katika makubaliano haya. Kwa hivyo, hizi ndizo sitakabadhi za kisheria zinazotumika kwa Nchi za Africa, kuhusiana na kulinda uhuru wa kuzungumza na haki za kupata habari. Mwongozo huu pia unajikita katika misimamo isiyokuwa ya makubaliano inayohusiana na haki hizi. Hii ni pamoja na *Uidhinishwaji wa Kanuni za Uhuru wa Kuzungumza na Upataji Habari Barani Africa,* ripoti za Ofisi ya Balozi kuhusu Haki za Binaadamu, ripotiza Ujumbe Maalum kuhusu uhuru wa kuzungumza na Uidhinishwaji wa Pamoja kuhusu Uhuru wa Kuzungumza na Mtandao uliotayarishwa na Ujumbe Maalumu wa UN kuhusu Uhuru wa Maoni na Kuzungumza, Mwakilishi wa Uhuru wa Habari katika Muungano la Usalama na Ushirikiano Europe (OSCE), Ujumbe Maalumu kuhusu Uhuru wa Kuzungumza katika Muungano Wa Mataifa ya America (OAS) na Ujumbe Maalumu kuhusu Uhuru wa Kuzungumza na Upataji wa Habari katika Tume ya Africa ya Haki za Kibinaadamu na Watu (Tume ya Africa.[5],

Katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na ongezeko la serikali barani ambao wameamua kuzima mtandao kabisa au kubana ufikiajia.

---

[1] Ripoti ya Frank La Rue, kuhusu uimarishaji na kulinda haki za uhuru wa maoni na kuzungumza, A/HRC/17/27, (2011), paras. 20-22. Angalia pia Tume ya Africa kuhusu Haki za Kibinaadamu na Watu, Uidhinishwaji wa Kanuni za Uhuru wa Kuzungumza na Upataji Habari Barani Africa, 65th Ordinary Session (21 Oktoba hadi tarehe 10 Novemba 2019), kanuni 37. Pia angalia *Amnesty International na wengine dhidi ya Togo*, ECOWAS Court of Justice, ECW/CCJ/APP/61/18 (tarehe 25 Juni 2020), unafikia kupitia https://www.accessnow.org/cms/assets/uploads/2020/07/ECOWAS_Togo_Judgement_2020.pdf.

[2] Angalia Kipengele 19.

[3] Angalia Kipengele 9.

[4] Angalia, kwa mfano, *Amnesty International na wengine dhidi ya Togo* ECW/CCJ/APP/61/18. Angalia pia UN Human Rights Committee, General Comment No. 34, Article 19: Freedoms of opinion and expression, UN Doc. CCPR/C/GC/34 (12 September 2011); Including General Comment No. 34, Kipengele 19: Uhuru wa Maoni na Kuzungumza, CCPR/C/GC/34, Julai 2011.

[5] Angalia Uidhinishwaji wa Pamoja kuhusu Uhuru wa Kuzungumza na Mtandao (tarehe 1 Juni 2011), accessible at https://www.osce.org/files/f/documents/e/9/78309.pdf.

Uzimaji mtandao, kwa kusudi la Mwongozo huu, inaweza kutajwa kuwa: "uvurugaji wa mtandao kimataifa au mawasiliano ya kielektroniki, inayolemaza ufikiaji au kutotumika inavyostahili kwa umati fulani au katika eneo, hususan kudhibiti mtiririko wa habari." [6] Aina ya vikwazo vinavyotumika ni pamoja na uzimaji kabisa, [7] ubanaji (kudorora kwa mtandao) na kuzuia majukwaa ya mawasiliano kama vile viunzi vya utumaji jumbe. Hali ya Uhuru wa Mtandao Barani Africa 2020[8] anasajili visa kadhaa vya aina hiyo kote barani. Hasa, Januari 2019, serikali ya Zimbabwe iliweka vikwazo kupata mtandao nchi nzima kwa wiki baada ya maandamano ya halaiki kupinga serikali. [9] Mnamo Julai 2020, serikali ya Ethiopia ilizima mtandao kwa wiki mbili baada ya maandamano ya watu waliotaka hatua ichukuliwe kufuatia kifo cha mwanamziki maarufu nchini humo. [10] Mnamo 2021 nchini Uganda na Zambia, serikali za nchi hizo zilizima mtandao kabla na baada ya uchaguzi mkuu wan chi hizo.[11] Vilevile, serikali ya Eswatini ilipiga marufuku utumiaji mtandao mara mbili mwaka 2021 kufuatia maandamano ya halaiki dhidi ya serikali.[12]

Uzimaji mtandao kwa kiwango unachangia pakubwa vizuizi katika uhuru wa kuzungumza na haki ya kupata habari, ambayo haikubaliki chini ya sheria za kimataifa kuhusiana na haki za binaadamu.[13]

Mwongozo huu hauangazii aina zote za vikwazo mtandaoni. Imebanwa kuangazia viwango muhimu vya kisheria kikanda na kimataifa ambavyo vitaorodheshwa na Mataifa kwa hali ambayo serikali zitakuwa zimeweka vikwazo vya aina yoyote vya uzimaji mtandao au uzuiaji wa kupata mtandao.

Uhuru wa kuzungumza na haki ya kupata habari vinahusiana na hutegemeana na haki nyinginezo za binaadamu, ikijumuisha, miongoni mwa, uhuru wa kujumuika, uhuru wa kukusanyika, haki ya kushirikia siasa na haki za faragha. Kwa kuongezea, uchumi, haki za kijamii na kitamaduni, ikiwa pamoja na haki za matibabu, inaweza kuhusishwa

[6] Huu ni ufafanuzi uliotayarishwa na AccessNow. Angalia https://www.accessnow.org/keepiton-faq/.
[7] Ambapo ufikiaji umekatwa kabisa.
[8] *Ripoti: Hali ya Uhuru wa Mtandao barani Africa 2020*, Ushirikiano kwa Sera Kimataifa za ICT katika Africa ya Mashariki na Kusini. https://cipesa.org/wp-content/uploads/2021/04/The-State-of-Internet-Freedom-in-Africa-2020-Report.pdf
[9] Angalia "Zimbabwe imezima mtandao huku wakikabili maandamano*" **kwenye** Al Jazeera*, 18 Januari 2019, inapatikana https://www.aljazeera.com/news/2019/1/18/zimbabwe-imposes-internet-shutdown-amid-crackdown-on-protests.
[10] Access Now, "Tumerudi hatarini: Ethiopia imezima mtandao tena", katika *Access Now*, 16 Julai 2020, inapatikana https://www.accessnow.org/back-in-the-dark-ethiopia-shuts-down-internet-once-again/.
[11] Nita Bhalla na Alice McCool, "Uzimaji mtandao nchini Uganda wakati wa uchaguzi", katika *Business Day,* 21 Januari 2021, inapatikana https://www.businesslive.co.za/bd/world/africa/2021-01-21-internet-shutdown-for-uganda-election/
[12] Access Now, "#KeepItOn: Serikali ya Eswatini yazima mtandao kupunguza maandamano", 21 Oktobar 2021, Inapatikana kwenye https://www.accessnow.org/keepiton-eswatini-protests/.
[13] Angalia maamuzi ya Korti ya Haki ya ECOWAS katika *Amnesty International kuhusu Togo & na wengine v The Togolese Republic* na katika *Registered Trustees of The Socio-Economic Rights & Accountability Project (SERAP) v Federal Republic of Nigeria*, ECW/CCJ/JUD/07/10 (30 Novemba 2010).

kuwa uwezo wa kupata au upataji huduma ya afya inategemea uwezo wa kufikia taarifa muhimu za afya.[14] Kwa kutumia uhuru wao wa kuzungumza, watu, binafsi au kwa ushirikiano na wengine, wanawajibisha serikali yao, vilevile kuchangia katika uandaaji wa sera za umma. Hii inahusiana na kudumisha haki za kushiriki siasa, iliyolindwa chini ya kipenge cha 25 cha ICCPR. Kwa kudumisha haki yao ya kupata habari, watu uweka kuwa wazi na kuwajibika. Kwa hivyo, uhuru wa kuzungumza na haki ya kupata habari ni haki muhimu ambazo lazima zilindwe kama njia ya kulinda sheria na haki nyinginezo za binaadamu.[15]

Mtandao kwa sasa umekuwa muhimu katika utumizi na kufurahikia uhuru wa kuzungumza na kupata habari, ilivyoidhinishwa na mamlaka mbalimbali ya UN na Ujumbe wa Africa. Ujumbe, katika kipengele cha Uidhinishaji wa Kanuni za Uhuru wa Kuzungumza na Upataji Habari, inahimiza Mataifa *"kutoa haki za uhuru wa kuzungumza na upataji habari mtandaoni na njia mwafaka za kudumisha haki hizi."*[16] Mtandao ni njia ya kupata habari na namna ya kuwasiliana na kutoa maoni yao kwa watu. Kupitia sababu hizi, Tume ya Africa kuhusu Haki za Kibinaadamu na Kiraia imedokeza kuwa:

> "Mataifa hayaingililia *haki za watu kutafuta, kupokea na kupitisha habari kupitia njia yoyote ya mawasiliano na teknolojia za mitandaoni…ila tu iwe uingiliaji huo umekubalika na kusawiana na sheria za haki za kibinaadamu na kanuni.*"

Baraza ya Haki za Binaadamu ya UN imefanya ugunduzi sawa.[17] Kamati ya Haki za Binaadamu ya UN, kwa kufafanua uwajibikaji wa Mataifa chini ya kipengele 19 cha ICCPR, inatoa misingi ya kuzuia haki kuhusiana na uhuru wa kuzungumza chini ya kipengele 10 cha ICCPR, pamoja na kufikia mtandao. Mataifa yanaweza kubania uhuru wa kuzungumza na haki ya kupata habari, iwapo ubaniaji huu umefafanuliwa kisheria;

---

[14] Kama Kamati ya Uchumi, haki ya Kijamii na Kitamaduni imesisitiza katika Maoni Jumla kuhusu Haki ya Afya, "haki ya afya ina uhusiano wa karibu na kutegemea uwepo wa haki nyingine za binaadamu, pamoja na haki za uhuru wa kupata habari". Angalia Maoni Jumla Nambari 14, UN Doc E/C.12/2000/4 (11 Agosti 2000), aya 3. Kupata habari inatambuliwa kila mahali katika Maoni Jumla kuwa kiungo muhimu katika uwepo wa hali mbalimbali ya haki ya afya.

[15] Angalia utangulizi na Kanuni 1 ya Tume ya Africa kwa Haki za Binaadamu na Raia, Uidhinishwaji wa Kanuni ya Uhuru wa Kuzungumza na Kupata habari barani Africa. Angalia pia Kamati ya Haki za Binaadamu ya UN, Maoni Jumla Nambari 34, aya 2 ambayoinasema: "Ni muhimu kwa jamii yoyote. Inajumuisha msingi imara wa kila jamii." Angalia pia Azimio 19/36, Haki za Binaadamu, demokrasia na utaratibu wa kisheria, UN Doc. A/HRC/RES/19/36 (19 Aprili 2012).

[16] Kanuni 37(1) ya Tume ya Africa kuhusu Haki za Binaadamu na Raia Uidhishwaji wa Kanuni ya Uhuru wa Kuzungumza na Habari barani Africa, 10 Novemba 2019.

[17] Angalia Azimio 44/12, Uhuru wa maoni na kuzungumza, UN Doc. A/HRC/44/L.18/Rev. (16 Julai 2020). Angalia pia Kamati ya Haki za Binadamu za UN, Maoni Jumla Nambario. 34; Ripoti ya Ujumbe Maalumu wa Kuimarisha na kulinda haki za uhuru wa maoni na kuzungumza (2011), aya 19-22.

Ina nia halali; na ni njia muhimu na ya sawa ili kufaulisha nia halali iliyokusudiwa.[18] taratibu sasa zipo katika Kanuni ya 9 ya Uidhinishwaji wa Kanuni za Uhuru wa Kuzungumza na Upataji Habari Africa iliyotumiwa na Ujumbe Wa Africa kufuata ufafanuzi wake wa kipengele 9 cha ACHPR.

Kuhiari kutumia uzimaji mtandao kama kigezo cha kudhalilisha uwajibikaji wa haki za kibinaadamu kufuatia dharura ya nchi, huenda isikubalike hata kama ni wakati wa dharura. Kipengele 4 cha ICCPR kinasema kuwa kulingana na dharura ya taifa ambayo inatishia maisha ya watu, Mataifa yatachukua hatua kidogo kutoka katika haki fulani, kama vile uhuru zakuzungumza na habari. Hata hivyo, hatua kama hizo ni za muda na sharti zilingane na hofu fulani za nchi.[19] Kufunga kabisa mifumo ya habari haiwezi kutosheleza masharti haya ya mahitaji na usawa.

Mwongozo huu hautaangazia hali za udhalilishwaji kulingana na dharura za umma. Itaangazia viwango hitajika kulingana na katika kipengele 19 cha ICCPR na kipengele 9 cha African Charter.

[18] Frank La Rue, Ripoti ya Ujumbe Maalum wa Kuimarisha na kulinda haki za uhuru wa maoni na kuzungumza (2011), aya 24.

[19] Angalia Kamati ya Haki za Binaadamu, Maoni Jumla Nambari 29, kipengele 4: Msamaha wakati wa Dharura, CCPR/C/21/Rev.1/Add.11 (31 Agosti 2001). Angalia pia Kanuni ya Siracusa kuhusu Vizuizi na Uwepo wa Msamaha katika makubaliano ya Kimataifa katika Haki za Kiraia na Kisiasa, pata kupitia https://www.icj.org/wp-content/uploads/1984/07/Siracusa-principles-ICCPR-legal-submission-1985-eng.pdf

**MWONGOZO WA KISHERIA**

## 1. Mataifa yana wajibu wa kuhakikisha haki za kibinaadamu zinadumishwa mtandaoni na pasipo mtandao.

| |
|---|
| Mataifa sharti yaheshimu, yalinde na yaimarishe haki zote za binaadamu, ikiwa na pamoja na uhuru wa kuzungumza, haki ya kupata habari na haki ya faragha kote mtandaoni na nje ya mtandaoni. |

***Maelezo***

Mataifa ya wajibu wa kuheshimu, kulinbda na kuimarisha haki zote mtandaoni sawa na nje ya mtandao. Hii ni pamoja na, hususan, uhuru wa kuzungumza, ambayo ni lazima bila mipaka na kupitia katika jukwaa lolote unalopendelea, kulingana na kipengele 19 cha Uidhinishwaji wa Kimataifa wa Haki za Binaadamu na kipengele 19 cha ICCPR.[20]

## 2. Vikwazo sharti viwekwe kufuata sheria (Kanuni ya Kisheria)

| |
|---|
| Vikwazo katika uhuru wa kuzungumza na habari, sharti viwekwe kisheria ambayo inalingana viwango vya haki za kimataifa za binaadamu. Vikwazo sharti visawiane na kanuni za kisheria, ambapo vimewekwa kufuata sheria na wazi, na maagizo ya kutumika kwake matokeo yake yanatabirika. |

***Maelezo***

i. Vizuizi katika upataji mtandao vinajumuisha vikwazo kwenye uhuru wa kuzungumza, na haki ya kupata habari. Kamati ya Haki za Binadaamu ya UN[21] na Ujumbe wa Africa[22] umethibitisha kuwa ili kuhakikisha uzingatiaji wa ICCPR na ACHPR hususani, vizuizi kama hivyo sharti viwekwe kwa kufuata sheria kulingana kanuni za sheria za kimataifa.

ii. Uamuzi wa kuweka vizuizi au vikwazo vyovyote katika kuingia mtandaoni sharti ufanywe tu na maafisa waliokubalika kisheria kuwa

[20] Angalia Azimio la Baraza la Haki za Binaadamu katika kukuza, kulinda na kufurahikia haki za binaadamu mtandaoni, A/HRC/38/7 (2018), aya. 1.

[21] Kamati ya Haki za Binaadamu ya UN, Maoni Jumla Nambari 34, aya 25 na 26.

[22] Angalia Tume ya Africa kuhusu Haki za Binaadamu na Kiraia, Uidhinishwaji wa Kanuni za Uhuru wa Kuzungumza na Upataji Habari barani Africa, kanuni 9 (1)(a).

na mamlaka kama hayo na maamuzi kama hayo sharti yafanywe baada ya kufuata taratibu zote zilizofafanuliwa kisheria.[23]

iii. Kamati Ya Haki Binaadamu[24] na Ujumbe wa Africa[25] umedokeza kuwa sheria inayotoa uwekaji wa vikwazo katika kupata mtandao huenda iliasiliwa kupitia utaratibu wa kawaida wa kisheria au mchakato wa mahakama inayolingana na sheria, na sharti iwe wazi kwa umma na kufikiwa.

iv. Inapotokea uamuzi unachukuliwa kuweka aina yoyote ya vikwazo katika uhuru wa kuzungumza, ikiwa pamoja uzimaji mtandao, serikali inayowajibika sharti iweke wazi vipengee fulani za sheria ambazo zimefaulisha na kuruhusu uwekaji vikwazo hivyo.[26]

## 3. Vikwazo vinaweza kuwekwa tu kulingana na makusudio halali.

Vizuizi katika uhuru wa kuzungumza na haki za kupata habari vinaweza kuwekwa kulingana na malengo ambayo tu yametambuliwa kihalali chini ya sheria za kimataifa: kwa kuweka usalama wa kitaifa, amri ya umma, afya ya umma, au maadili, au kulinda haki au maadili yaw engine.

***Commentary***

i. Kipengele 19(3) cha ICCPR kinatoa hatima na maamuzi kamilifu ambapo uhuru wa kuzungumza na habari huweza kubanwa, na ni (i) kwa kulinda haki au mienendo ya wengine, au (ii) kwa kulinda usalama wa taifa au amri ya umma, au ya afya ya raia au maadili. Vikwazo kwa upataji wa mtandao, ikiwa pamoja na uzimaji mtandao haifai kuwekwa kwa makusudia yaliyo kinyume na haya yametajwa.[27]

ii. Wakati uamuzi wowote umechukuliwa kuweka vikwazo vyovyote dhidi ya kutumia mtandao, ikiwa ni pamoja na kupata mtandao, serikali husika sharti itoe sababu halali kuhusiana ni kwa ni nini wakachukua hatua ya kuweka vikwazo hivyo.

[23] Angalia Kamati ya Haki za Binaadamu ya UN, Maoni Jumla Nambari 34.
[24] Kamati ya Haki za Binaadamu ya UN, Maoni Jumla Nambari 34, aya 24.
[25] Angalia Tume ya Africa kuhusu Haki za Binaadamu na Kiraia, Uidhinishwaji wa Kanuni za Uhuru wa Kuzungumza na Upataji Habari barani Africa, kanuni 9(2).
[26] Angalia *Korneenko et al. v. Belarus*, Mawasiliano ya Kamati Haki za Binaadamu Nambari 1553/2007, maoni yalidumishwa 20 Machi 2009, UN Doc. CCPR/C/95/D/1553/2007 (HRC2009).
[27] Kipengele 19(3) cha ICCPR.

iii. Mamlamka inayohusika sharti ibainishe kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kuzima kwa mtandao na kupunguza ama kushughulikia tatizo lililotambulika dhidi ya lengo halali.[28]

## 4. Vizuizi kuhusu haki za kibinadamu hazifai kubagua mtu kwa misingi ya ngozi, rangi, hali ya kimapenzi pendelewa au utambulisho wa jinsia, umri, jinsia, dini, lugha ya kisiasa ama maoni mengine, uraia, utaifa ama uhamiaji, taifa, jamaa au asili yako, ukoo, hali ya kiafya, ulemavu, mali, hali yako ya kijamii na kiuchumi, kuzaliwa ama vigezo vingine.

***Maelezo***

| |
|---|
| Any Vikwazo vyovyote vya haki za kibinadamu, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na uhuru wa kujieleza na haki ya kupata habari, sharti katika kusudio lao, itengeneze na utekelezwaji isibague kwa misingi ya makundi, rangi, hali ya kimapenzi anayoegemea au utambulisho wa kijinsia, umri, jinsia, dini, lugha ya kisiasa ama maoni mengine, uraia ,utaifa ama hali ya uhamiaji, taifa, asili yako au kijamii, ukoo, hali ya kiafya, ulemavu, mali, hali ya kiuchumi, na kijamii, uzao, au vigezo vingine. |

i. Katika kipengele cha 2(1), 3 na 26 cha makubaliano kuhusu haki za kiraia na kisiasa, ICCPR, Mataifa yana wajibu kuhakikisha kuwa haki zinazopatikana katika Makubaliano huo ikiwa ni pamoja na uhuru wa kujieleza na kupata taarifa, zinapatikana na kutumika na kila mmoja katika eneo lake na walio chini yao bila ubaguzi. Vizuizi vinavyobagua mtu yeyote katika misingi yoyote isoyokubalika iko kinyume na Kanuni hizi. Kipengele cha 26 cha Makubaliano hayo kinatumika pakubwa, si tu katika haki zisizobaguzi za ICCPR, bali kuzingatia Hulka zote za Taifa. Hususan, kipengele 26 kinasema kwamba: "*Watu wote wako sawa chini ya sheria na wanafaa bila ubaguzi kupata haki ya ulinzi ya sheria hizo. Kwa kuzingatia hili, sheria itazuia ubaguzi wa aina yoyote na kuhakikisha kuwa watu wote wanapata haki sawa katika utekelezwaji wa kisawasawa katika ulinzi dhidi ya ubaguzi kwa misingi ya rangi, lugha, dini, lugha ya kisiasa ama maono mengine, taifa ama jamii mtu anakotoka, mali yake, kuzaliwa ama vigezo vingine.*"[29]

---

[28] Kamati Ya Haki za Binaadamu ya UN, Maoni Jumla Nambari 34, aya 35.

[29] Wajibu huu pia umeandikwa katika mikataba mingine ikiwa pamoja na Mkataba wa Kimataifa kuhusu Uondoaji wa Aina zote dhidi ya Wanawake. Angalia pia Tume ya Kimataifa ya Wanasheria, "The Tunis Declaration on

ii. Article Kipengele cha 2 cha ACHPR[30] kinazungumzia wajibu sawa na huo wa kutokuwa na ubaguzi.

iii. Huku ICCPR na ACHPR ikiorodhesha hali fulani kwa misingi ambayo ubaguzi haukubaliki, kuna hali ya jumla ya "vigezo vingine" imejumuishwa pia. Ukuaji wa sasa katika sheria za kimataifa umefanikiwa kupata misingi mingine mingi ambayo imejumuishwa katika huu mkataba. Kamati ya Haki ya Binaadamu ya UN na Kamati ya Uchumi, Haki za Jamii na Kitamaduni zimethibitisha hili katika sheria zake.[31]

iv. Vizuizi kuhusu kutumia mtandao, ikijumuisha kuzima kwa mtandao kwa watu binafsi au makundi yanayolengwa chini ya misingi yote iliyoorodheshwa inachukuliwa kama kuvunja kwa sheria hizi.[32] Vizuizi vya mtandao ambavyo viko moja kwa moja ama visivyo vya moja kwa moja ama vinadhihirisha ubaguzi katika misingi yoyote haiambatani na sheria za haki za kibinadamu za kimataifa.

## 5. Vizuizi vitawekwa tu iwapo ni lazima.

| |
|---|
| Hatua ambazo zinajumuisha vizuizi kwenye uhuru wa kujieleza na haki ya kupata habari inaweza kuwekwa tu kama ni lazima kwa kulinda haki. |

***Maelezo***

i. Article Kifungu cha 19(3) cha ICCPR kinatoa mipaka ya uhuru wa kujieleza na haki ya kupata habari inaweza kuwekwa tu ikiwa ni muhimu kulinda au kufanikisha mojawapo ya makusudi ya lioorodheshwa. Ikiwa sio lazima na ikiwa njia zingine zisizo na kikomo zinaweza kupitishwa na kutekelezwa kwa madhumuni, kizuizi hakitapitishwa kuwa inaruhusiwa. Katika kufafanua upeo wa kifungu hiki, Kamati ya

---

Kuimarisha Utawala wa Sheria na Haki za Binadamu" (Machi 2019), aya. 44, inapatikana kwa https://www.icj.org/wp-content/uploads/2019/04/Universal-ICJ-The-Tunis-Declaration-Advocacy-2019-ENG.pdf .

[30] Inasema kwamba, "[e] kila mtu atastahiki kufurahia haki na uhuru unaotambuliwa na kuhakikishwa katika Mkataba huu bila ubaguzi wa aina yoyote kama vile rangi, kabila, rangi, jinsia, lugha, dini, siasa au maoni mengine yoyote, asili ya kitaifa na kijamii, bahati, kuzaliwa au hadhi nyingine.

[31] Angalia, kwa mfano, Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni, Maoni ya Jumla Na. 20, Kutobagua katika haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni, UN Doc CCPR/C/GC/37 (20 Septemba 2020)

[32] Angalia Ripoti ya Mwandishi Maalum kuhusu ukuzaji na ulinzi wa haki ya uhuru wa maoni na kujieleza,

(2011)

Haki za Binaadamu[33] imesisitiza kwamba uhusiano wa moja kwa moja lazima uthibitishwe kuwepo kati ya kizuizi kilichowekwa na tishio dhidi ya madhumuni halali ambayo kizuizi kinataka kushughulikia. Vile vile, Tume ya Afrika imethibitisha kwamba ili kukidhi matakwa ya ulazima, ukomo wa uhuru wa kujieleza "utatokana na hitaji kubwa na kubwa ambalo ni muhimu na la kutosha" kutishia kusudi halali.[34]

ii. Vizuizi vya ufikiaji wa mtandao, vinaweza kuwekwa tu ambapo vizuizi kama hivyo ni muhimu sana na kwa dhahiri ili kulinda au kufikia madhumuni halali yaliyotajwa. Kuzima kabisa kwa mtandao kuna uwezekano kuwa kamwe kuwa kipimo cha lazima au sawia. Kama Kamati ya Haki za Binadamu ilivyothibitisha:

"*Vizuizi vyovyote vya uendeshaji wa tovuti, blogu au mfumo mwingine wowote wa kusambaza taarifa unaotegemea mtandao, kielektroniki au mwingine kama huo, ikiwa ni pamoja na mifumo ya kusaidia mawasiliano hayo, kama vile watoa huduma za intaneti au injini ya utafutaji, inaruhusiwa tu kwa kiwango ambacho sambamba na aya ya 3 [kuweka msingi halali wa vikwazo]. Vikwazo vinavyoruhusiwa kwa ujumla vinapaswa kuwa mahususi kwa maudhui; marufuku ya jumla juu ya uendeshaji wa tovuti na mifumo fulani haiendani na aya ya3.*[35]

iii. Mamlaka inayoweka vikwazo kwenye mtandao lazima ionyeshe kwamba kuna uhusiano wa moja kwa moja na wa haraka kati ya kuzima mtandao na tishio ambalo uzuiaji huo unalenga kushughulikia, na kwamba kizuizi hicho ni muhimu sana ili kukidhi tishio.

## 6. Uwiano

### a. Vikwazo lazima viwe njia ndogo zaidi za kuweka vikwazo

| |
|---|
| Vizuizi juu ya uhuru wa kujieleza na haki ya kupata habari lazima iwe njia isiyo na vikwazo zaidi ya kulinda madhumuni halali yaliyotajwa. |

***Maelezo***

[33] Kamati ya Haki za Kibinadamu ya Umoja wa Mataifa, Maoni ya Jumla Na. 34, aya. 35.

[34] Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Tamko la Kanuni za Uhuru wa Kujieleza na Kupata Habari Barani Afrika, kanuni ya 9(4).

[35] Kamati ya Haki za Kibinadamu ya Umoja wa Mataifa, Maoni ya Jumla Na. 34, aya. 44 na 45.

i. Kamati ya Haki za Kibinadamu ya Umoja wa Mataifa[36] na Tume ya Afrika ya Haki za Kibinadamu[37] zimebainisha kuwa vikwazo vya utumiaji wa uhuru wa kujieleza lazima visiweke hatarini kiini cha haki yenyewe. Vyombo vyote viwili vimetoa maoni zaidi kwamba vizuizi lazima viwe vyombo visivyoingilia kati vya vile ambavyo vinaweza kufikia kazi sawa ya ulinzi"[38]

ii. Kwa hivyo, pale ambapo imekuwa muhimu kuweka vizuizi vya ufikiaji wa mtandao, mamlaka inayohusika lazima ichague na kutumia njia zenye vizuizi vidogo zaidi vya kufikia au kulinda madhumuni halali yaliyotajwa. Kuzima kwa mtandao kunaweza tu kuwekwa ikiwa ni njia ndogo zaidi ya kufikia kazi ya kinga iliyoelezwa.

## b. Vikwazo lazima visiwe vya kupita kiasi

| |
|---|
| Vizuizi vya uhuru wa kujieleza na haki ya kupata habari lazima visiwe vya kupita kiasi |

***Maelezo***

i. Kamati ya Haki za Binaadamu ya UN[39] imebainisha kwamba pale ambapo vikwazo vya uhuru wa kujieleza na haki ya kupata habari ni muhimu ili kuendeleza madhumuni halali, mamlaka inayohusika lazima ihakikishe kwamba vikwazo hivyo vinajengwa kwa uangalifu.[40] Upeo, ukubwa na namna ya utekelezaji wa vikwazo lazima uandaliwe kwa uangalifu ili kupunguza athari zao kwa kile ambacho ni muhimu sana na uwiano kwa ajili ya ulinzi wa madhumuni halali yanayohusika.

ii. Restrictions vya ufikiaji wa mtandao, ikiwa ni pamoja na kuzima kwa mtandao, ni lazima kulengwa iwezekanavyo ili kuzuia kuingiliwa kwao na haki za watu wote walio chini ya mamlaka ya Serikali, ambayo Serikali inalazimika kuheshimu na kulinda. Kwa asili yake, kusimamishwa kwa jumla kwa mtandao lazima kuwe na athari sawa

[36] Kamati Ya Haki za Binaadamu ya UN, Maoni Jumla Nambari34, aya 21.
37 Tume ya Afica kuhusu Haki za Binaadamu na Raia, Uidhinishwaji wa Kanuni za Uhuru wa Kuzungumza na Haki ya Kupata Habaribarani Africa, kanuni 9(4)(b).
38 Ibid, Kanuni ya 9(4) (b). Tazama pia Kamati ya Haki za Kibinadamu ya Umoja wa Mataifa, Maoni ya Jumla Na. 34, aya. 34.
39 Kamati ya Haki za Kibinadamu ya UN, Maoni ya Jumla Na. 34, aya. 34.
40 Ibid, aya. 28.

kwa wanachama wa umma na kwa hivyo kutatokea mwitikio usio na uwiano isipokuwa mamlaka husika inaweza kuonyesha kwamba vikwazo hivyo ndiyo njia pekee inayopatikana ya kulinda lengo halali lililotishiwa.[41]

iii. Vikwazo kwenye kupata mtandao, ikijumuisha kuzima mtandao, hata kama inakubalika, itawekwa tu kwa muda mfupi na wakati ulio wazi ambao ni lazima kwa kulinda lengo lililokusudiwa kulingana na uhalali wake.

c. Mamlaka ya kuweka vikwazo sharti yadhibitiwe

> Mamlaka ya kufafanua vikwazo sharti idhibitiwe kisheria na kwa mfumo na kusimamia, ikiwa pamoja na uangalizi wa majopo huru ya mahakama na utawala.

***Maelezo***

i. Sheria inayoidhinisha uwekaji wa vikwazo vya uhuru wa kujieleza na haki ya kupata habari lazima ibainishe kwa uwazi mamlaka zilizopewa mamlaka ya kuweka vikwazo hivyo, mazingira ambayo vikwazo vinaweza kuwekwa, aina maalum ya vikwazo vinavyoweza kuwa. zilizowekwa na taratibu zinazopaswa kufuatwa wakati wa kutumia nguvu hizo za vikwazo.[42]

ii. Sheria inayoidhinisha kuzima kwa mtandao lazima ibainishe wazi mamlaka ambayo inaweza kutumia mamlaka kama hayo. Uwezo mahususi wa kufanya hivyo unapaswa kutolewa katika sheria, na si tu katika sheria za utawala au amri za utendaji. Sheria lazima ionyeshe wazi kwamba kuzima kwa mtandao ni kipimo cha kizuizi cha hatua ya mwisho, ambayo itafanywa tu chini ya hali zilizoainishwa katika sheria. Sheria lazima ieleze aina au asili ya kukatika kwa mtandao ambayo inaweza kuwekwa pamoja na kuagiza muda wa juu zaidi wa kusimamishwa kwa mtandao

iii. Sheria iliyotungwa kuidhinisha kuzimwa kwa mtandao lazima iweke wazi taratibu za kufuatwa kabla ya vikwazo hivyo kuwekwa. Taratibu hizo zijumuishe maombi ya hati ya mahakama kutoka kwa mahakama yenye uwezo. Wakati wa kuhukumu maombi ya kibali cha kuweka vizuizi vya mtandao, mahakama hakikisha kwamba

---

[41] Tume ya Afica kuhusu Haki za Binaadamu na Raia, Uidhinishwaji wa Kanuni za Uhuru wa Kuzungumza na Haki ya Kupata Habaribarani Africa, kanuni 38(2).

[42] Kamati ya Haki za Kibinadamu ya UN, Maoni ya Jumla Nambari 34, aya 25.

mahitaji ya uhalali, madhumuni halali, kutobagua, ulazima na uwiano (yaliyoainishwa katika aya ya 4-6 ya Mwongozo huu) yanatimizwa vya kutosha. Wale ambao vikwazo vinaelekezwa kwao, mawakili wao na washikadau wengine walioathirika lazima wapewe fursa ya kutoa uwakilishi.

iv. Uamuzi halisi wa kuzima mtandao unapaswa kufanywa tu na mtu aliyeidhinishwa baada ya kufuata taratibu zote zilizowekwa.

## 7. Vikwazo sharti view chini ya uangalizi wa mahakama

Vikwazo vya haki za binaadamu, vikiwa pamoja na vizuizi vya uhuru wa kuzungumza na haki ya kupata habari view chini ya uangalizi wa mahakama.

***Maelezo***

i. Kipengele cha 2 (3) cha ICCPR, kinazitaka Mataifa kuweka taratibu zinazofaa za mahakama na kiutawala kwa ajili ya kushughulikia madai ya ukiukaji wa haki chini ya sheria za ndani.[43]

ii. Vikwazo dhidi ya kupata mtandao inajumuisha uzuiaji wa haki za binaadamu ikiwa pamoja na uhuru wa kuzungumza. Vizuizi hivyo lazima vipitiwe upya na mahakama huru na isiyopendelea upande wowote, kwa kuwa, kama ilivyobainishwa na Kamati ya Haki za Kibinadamu, ulinzi wa haki unahusisha wajibu wa mamlaka ya mahakama.[44]

iii. Upigaji marufuku wa kuingia mtandaoni ina uwezekano wa kuvuruga na athari mbaya dhidi ya haki za bianaadmu. Kwa hivyo, maombi ambayo yanapinga ufaafu wa kuzima kwa mtandao lazima yapewe kipaumbele.

iv. Wakati wa kuhakiki uhalali wa vikwazo dhidi ya kupata mtandao, ikiwa pamoja na kuzimwa kwa mtandao. Mahakama zitazingatia iwapo vikwazo vilivyopingwa vinakidhi viwango vya uhalali, kutobagua, umuhimu na uwiano, kulingana na aya ya 4-7 ya Mwongozo huu hapo juu. Baada ya mapitio, mahakama itatoa suluhu zenye ufanisi kushughulikia ukiukaji uliosababishwa

[43] Angalia Kamati ya Haki za Binaadamu ya Umoja wa Mataifa, Maoni Jumla Nambari 31, Hali ya Wajibu Jumla wa Kisheria Unawekwa dhidi ya Mataifa Wanachama ambao ni Washirika wa Mkataba, UN Doc. CCPR/C/21/Rev.1/Add.13 (26 Mei 2004) aya 15.
[44] Ibid.

na vikwazo vyovyote vya upatikanaji wa intaneti ambavyo havikidhi viwango hivi.[45]

## 8. Upataji wa fidia imara na marekebisho sharti yawepo ili kushughulikia tishio na kufidia kwa ukiukaji sheria.

| |
|---|
| Kila mtu ana haki ya kupata suluhu na fidia inayotokana na ukiukwaji wa haki, ikiwa ni pamoja na ukiukwaji wa uhuru wa kujieleza unaotokana na kizuizi kisicho halali cha ufikiaji wa mtandao. |

***Maelezo*** [46]

i. Chini ya Kipengele 2(3)(a) na (c) cha ICCPR, Nchi zina wajibu wa kuhakikisha kwamba ufikiaji wa suluhisho na fidia madhubuti inatolewa kwa mtu yeyote aliye chini ya mamlaka ya serikali ambaye haki zake zinakiukwa au kutishiwa, na kuhakikisha kwamba maagizo ya fidia yanatekelezwa vya kutosha.

ii. Ilivyoelezwa katika *Kanuni Msingi na Miongozo kuhusu Haki ya Fidia,* fidia ya uvunjaji wa sheria za haki za binaadamu za kimataifa za mwathiriwa ni pamoja na haki za (a) upataji haki sawa na kamilifu; (b) fidia ya kutosha, yenye ufanisi na ya haraka kwa madhara yaliyotokea; (c) kupata taarifa muhimu kuhusu ukiukwaji na taratibu za ulipaji fidia.[47]

iii. Ili kuonekana kuwa kamilifu, fidia sharti iwe na uwezo wa kufidia haki iliyokiukwa kadri iwezekanavyo, kusitisha ukiukaji unaoendelea na kuzuia urudiaji wa ukiukaji kama huo siku za baadaye.[48]

iv. Pahali pana marekebisho ya kufidia ukiukaji unaotokana na vikwazo haramu vya kupata mtandao, hesabu ya fidia sharti iwe kamili,

[45] Tazama kwa mfano, uamuzi wa Mahakama ya Haki ya ECOWAS katika Amnesty International Togo & Others v Jamhuri ya Togo ambapo Mahakama ilipata kwamba kwa kuzima mtandao mwaka wa 2017, Serikali ilikiuka haki za walalamikaji, ikiwa ni pamoja na haki yao ya uhuru. ya kujieleza na kupata habari. Mahakama ilitoa fidia kwa walalamikaji na kuamuru Togo kuweka mfumo wa kisheria unaolinda uhuru wa kujieleza unaoendana na viwango vya sheria za kimataifa za haki za binadamu. Mahakama pia iliamuru Togo kutofunga mtandao tena.

[46] Kwa uchanganuzi wa kina wa haki ya suluhu yenye ufanisi na fidia chini ya sheria ya kimataifa, ona Tume ya Kimataifa ya Wanasheria, "Haki ya Marekebisho na Matengenezo ya Haki za Jumla za Kibinadamu Ukiukaji: Mwongozo wa Practitioner 2" (Toleo Lililorekebishwa, Novemba 2018), linapatikana katika https://www.icj.org/the-right-to-a-remedy-and-reparation-for-gross-human-rights-violations-2018-sasisha-mwongozo-no-2/.

[47] Kanuni na Miongozo ya Msingi kuhusu Haki ya Kutatuliwa na Fidia kwa Waathiriwa wa Ukiukaji Mkubwa wa Sheria ya Kimataifa ya Haki za Kibinadamu na Ukiukaji Mbaya wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu, Hati ya Umoja wa Mataifa. A/RES/60/147 (16 Desemba 2005), aya. 11.

[48] Kamati ya Haki za Kibinadamu ya Umoja wa Mataifa, Maoni ya Jumla Na. 31, aya. 15 – 19

ya haraka na iliyo sawa kina cha ukiukaji huo na uharibifu uliosababishwa.[49]

v. Katika hali fulani Nchi lazima ziweke na kutekeleza hatua za muda ili kuepuka ukiukaji unaoendelea unaosababishwa na kuzima kwa mtandao, na kujitahidi kurekebisha haraka iwezekanavyo madhara yoyote kwa haki za binadamu ambayo yanaweza kuwa yamesababishwa na ukiukwaji huo.[50]

## 9. Mbinu za uangalizi wa kiutawala

| |
|---|
| Vizuizi katika haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na vikwazo vya uhuru wa kujieleza na haki ya kupata habari lazima iwe chini ya usimamizi wa vyombo huru vya utawala au mahakama ili kuhakikisha uwazi na uwajibikaji. |

***Maelezo***

i. Kamati ya Haki za Kibinadamu ya[51] na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Watu[52] zimebainisha kuwa Mataifa lazima yaanzishe mifumo huru ya kiutawala na isiyoegemea upande wowote ili kutoa uangalizi juu ya utekelezaji au utekelezaji wa majukumu ya kuheshimu, kulinda, kukuza na kutimiza haki za binadamu.

*ii.* Kulingana na haki za faragha, ambayo pia inaweza kukiukwa kwa kuweka vikwazo vya mtandao, Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Kibinadamu ametoa maoni[53] kwamba *"kufurahia haki ya faragha kunategemea kwa kiasi kikubwa mfumo wa kisheria, udhibiti na kitaasisi ambao hutoa, ulinzi wa kutosha, ikijumuisha mbinu madhubuti za uangalizi."*

iii. Pamoja na kuhakikisha kuwa korti huru zisizo na mapendeleo zinashughulikia ukaguzi wa vikwazo kwenye upataji mtandao, Mataifa pia sharti yaunde vyombo vya utawala vilivyo huru na vyenye rasilimali za kutosha (kama vile taasisi za kitaifa za haki za binadamu)

[49] Kanuni za Msingi na Miongozo ya Haki ya Kupata Tiba, aya. 15.

[50] Kamati ya Haki za Kibinadamu ya Umoja wa Mataifa, Maoni ya Jumla Na. 31, aya. 19.

[51] Ibid.

[52] Tazama Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Tamko la Kanuni za Uhuru wa Kujieleza na Upatikanaji wa Taarifa katika Afrika, kanuni 9(2)(b) na 34(1) .

[53] Ripoti ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Kibinadamu: Haki ya faragha katika enzi ya kidijitali, UN Doc. A/HRC/39/29 (3 Agosti 2018), para.26.Basic Principles and Guidelines on the Right to a Remedy, para. 15.

ambayo hufuatilia na kutoa uangalizi juu ya uwekaji na utekelezaji wa vikwazo vya mtandao.[54]

iv. Wanachama wa kiutawala wa majopo ya uangalizi sharti wateuliwe kwa uwazi, bila mapendeleo ambapo utahakikisha uwezo wao wa kufanya kazi bilakuingililiwa.

v. Majopo kama hayo sharti yawe na uwezo wa kupokea na kuchunguza malalamishi ya ukiukaji haraka nay yawe na uwezo wa kutoa fidia na suluhu imara.[55] Vile vile vinapaswa kuwa na uwezo wa kuanzisha uchunguzi kwa hiari yao wenyewe, ili kubaini usahihi wa vikwazo vya mtandao vilivyowekwa.

vi. Inapaswa kuwa lazima kwa mashirika yote ya Serikali na kila mtu kushirikiana na shirika la uangalizi wakati wa kufanya uchunguzi wake kuhusu vikwazo vya mtandao.

vii. Wakati wowote uamuzi wa kuweka vikwazo vya upatikanaji wa mtandao unapowekwa, ikiwa ni pamoja na kuzima mtandao, mamlaka inayohusika na kuweka vikwazo inapaswa kutoa taarifa mara moja kwa umma na chombo husika cha uangalizi, pamoja na kufichua madhumuni halali yaliyotolewa na vikwazo na muda uliokusudiwa wa vikwazo.

## 10. Biashara zote, zikiwemo kampuni za kibinafsi za mawasiliano, lazima ziheshimu haki za binadamu mtandaoni na nje ya mtandao..

| |
|---|
| Mashirika ya Biashara sharti yaheshimu haki za binaadamu, ikiwa ni pamoja na uhuru wa kujieleza, haki ya faragha na upataji habari mtandaoni, na sharti wasite kuweka vikwazo kinyume cha sheria na ambavyo havilingani na viwango hitajika, usawa na bila-ubaguzi. |

***Maelezo***

i. Business Mashirika ya kibiashara yana wajibu wa kuheshimu haki za binadamu. Lazima yaepuke kukiuka haki za binadamu za wengine na vilevile yashughulikie athari za haki zabinadamu zinazotokana nao. [56] Kampuni za kibinafsi zinazotoa huduma za mawasiliano ya simu zina wajibu wa kuheshimu

[54] Angalia kanuni 17(1) za Tume ya Africa kuhusu Haki za Binaadamu na Kiraia kwa Uidhinishwaji wa Kanuni za Uhuru wa Kujieleza na Upataji wa Habari barani Africa, ambayo inasema "Mamlaka ya udhibiti ya umma ambayo yanatumia mamlaka katika sehemu za utangazaji, mawasiliano au miundomsingi ya mtandao yatalindwa kikamilifu dhidi ya uvurugaji wa kisiasa, kibiashara au namna nyingine."

[55] Kamati ya Haki za Binaadamu ya UN, Maoni Jumla Nambari 31, aya 15.

[56] Kanuni za Mwongozo wa Biashara na Haki za Binaadamu: Kutekeleze mifumo "Heshima na Fidia" ya Umoja wa Mataifa, UN Doc. A/HRC/17/31 (21 Machi 2011), kanuni 11.

uhuru wa mtandao, ikiwa ni pamoja na kutekelezwa kwa uhuru wa kujieleza, haki ya kupata habari na uhuru wa kimtandao. Ni lazima zijiepushe dhidi ya kuweka vikwazo mtandaoni ambavyo havijaidhinishwa kisheria, na ambavyo havikidhi viwango vya umuhimu, uwiano na kutobagua kama ilivyobainishwa katika aya ya 4-7 ya Mwongozo huu.

ii. Kulingana na *Kanuni za Mwongozo wa UN kuhusu Biashara na Haki za Binaadamu (UNGPs)*,[57] kuasiliwa na Baraza la Haki za Binaadamu la UN 2011, ili kutimiza wajibu wao wa kuheshimu haki za binadamu, mashirika ya biashara yanapaswa kuwa na sera na mipango inayojumuisha: (a) kuwajibika kisera ili kutimiza wajibu wao wa kuheshimu haki za binadamu (b) mchakato wa uchunguzi wa haki za binadamu ili kutambua, kuzuia, kupunguza na kutoa hesabu kuhusu jinsi wanavyoshughulikia athari zao katika haki za binadamu na (c) michakato ya kuwezesha kutatua athari zozote mbaya za haki za binadamu wanazosababisha au wanazochangia. Kampuni za kibinafsi zinazotoa huduma za mawasiliano ya simu sharti, ziwe na sera za uwajibikaji zilizoandikwa kuongoza katika kuheshimu uhuru wa mtandao, na lazima zifanye bidii zinapopokea maagizo ya kuweka vikwazo vya mtandao.

iii. Kufanya umakini unahusisha kuhakikisha kuwa amri zinatolewa kisheria kulingana na haki za binaadamu, ambazo zimetolewa na watu ambao wamehitimu kisheria kutoa amri kama hizo, zinatolewa kulingana na utaratibu uliopo kwenye sheria na kwamba vikwazo vinavyowekwa vinazingatia vigezo vya ulazima, uwiano na kutobagua kama ilivyoelezwa katika aya ya 4-7 ya Mwongozo huu.

iv. Ikitokea kwamba amri za kuweka vikwazo hazizingatii viwango hivi na ni kinyume cha sheria, kampuni za kibinafsi zinahitajiwa kuchukua hatua za kulinda uhuru wa mtandao na hatua hizo ni pamoja na kukataa kufuata amri zisizo halali na kuwasilisha amri hizo mahakamani. Kampuni sharti ziwe wazi na zifichue kwa umma zinapopokea maagizo yasiyo halali ya kuweka vikwazo vya mtandaoni.

v. Kwa watu wanaolalamika kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu, kampuni lazima zitoe mbinu za kurekebisha kupitia njia zinazoendana, ila zisibadili nafasi ya taratibu za mahakama na nyinginezo.

[57] Kanuni za Mwongozo za UN kuhusu Biashara na Haki za Binaadamu, kanuni 15.

vi. As Kama Kanuni ya 29 ya UNGPs inavyoweka, "ili kuwezesha malalamishi kushughulikiwa mapema na kusuluhishwa moja kwa moja, kampuni za biashara zinapaswa kuanzisha au kushiriki katika mifumo madhubuti ya kushughulikia ya malalamishi kwa watu binafsi na jamii ambazo zinaweza kuathiriwa vibaya." UNGPs vilevile huweka viwango vya chini vya utaratibu wa malalamishi yasiyo ya kimahakama, ambavyo nihusisha hitaji la kuwa ni halali, kufikiwa, kutabirika, usawa, uwazi, kuendana na haki-za uwiano na katika ushirikiano na mazungumzo.[58]

[58] Kanuni za Mwongozo za UN, kanuni 31. Angalia pia Tume ya Kimataifa ya Wanasheria, “Operereshini Kamilifu- Mbinu Sawa ya Malilio” (Novemba 2019), inapatikana https://www.icj.org/companies-around-the-world-must-do-more-to-ensure-effective-operational-grievance-mechanism-practices-and-provide-clear-and-transparent-information/.

## Wanachama wa Tume

Machi 2021 (kwa orodha kamili, tafadhali pitia www.icj.org/commission)

**Rais:**

Prof. Robert Goldman, United States

**Makamu-Rais:**

Prof. Carlos Ayala, Venezuela

Justice Radmila Dragicevic-Dicic, Serbia

**Kamati Kuu:**

Justice Sir Nicolas Bratza, UK

Dame Silvia Cartwright, New Zealand (Chair)

Justice Martine Comte,France

Ms. Nahla Haidar El Addal, Lebanon

Mr. Shawan Jabarin,Palestine

Ms. Mikiko Otani, Japan

Justice Sanji Monageng, Botswana

MrBelisáriodosSantosJúnior,Brazil

Prof. Marco Sassòli – Italy/Switzerland

Ms. Ambiga Sreenevasan –Malaysia

**Other Commission Members:**

ProfessorKyong-WahnAhn,RepublicofKorea Justice
Chinara Aidarbekova,Kyrgyzstan

Justice Adolfo Azcuna, Philippines Ms
Hadeel Abdel Aziz, Jordan
Mr Reed Brody, United States Justice
Azhar Cachalia, South Africa Prof. Miguel
Carbonell, Mexico Justice Moses
Chinhengo,Zimbabwe Prof. Sarah
Cleveland, United States Justice Martine
Comte,France
Mr Marzen Darwish, Syria Mr
Gamal Eid, Egypt
Mr Roberto Garretón, Chile
Ms Nahla Haidar El Addal, Lebanon Prof.

Michelo Hansungule, Zambia Ms Gulnora

Ishankanova,Uzbekistan

Ms Imrana Jalal, Fiji
Justice Kalthoum Kennou, Tunisia
Ms Jamesina Essie L. King, Sierra Leone

Prof. César Landa, Peru Justice
Ketil Lund, Norway
Justice Qinisile Mabuza, Swaziland Justice

José Antonio Martín Pallín, Spain Prof. Juan

Méndez, Argentina

Justice Charles Mkandawire,

Malawi Justice Yvonne Mokgoro,

South Africa Justice Tamara

Morschakova, Russia

Justice Willly Mutunga, Kenya
Justice Egbert Myjer,
Netherlands
Justice John Lawrence O'Meally, Australia

Ms Mikiko Otani, Japan
Justice Fatsah Ouguergouz,
Algeria Dr Jarna Petman,
Finland
Prof. Mónica Pinto, Argentina
Prof. Victor Rodriguez Rescia, Costa Rica

Mr Alejandro Salinas Rivera,
Chile Mr Michael Sfard,Israel
Prof. Marco Sassoli,
Italy-Switzerland Justice Ajit
Prakash Shah, India Justice
Kalyan Shrestha,Nepal
Ms Ambiga Sreenevasan,
Malaysia Justice Marwan
Tashani, Libya
Mr Wilder Tayler,
Uruguay Justice Philippe
Texier, France
Justice Lillian Tibatemwa-Ekirikubinza,

Uganda Justice Stefan Trechsel,
Switzerland
Prof. Rodrigo Uprimny Yepes, Colombia

International
Commission
of Jurists
P.O. Box 91
Rue des Bains 33
CH 1211 Geneva 8
Switzerland

**t** +41 22 979 38 00
**f** +41 22 979 38 01
www.icj.org